
AFISI YA MKUU WA MASHTAKA YA UMMA

# OMBI LA KUJADILIANA KUHUSU KESI






Mwendesha mashtaka ya umma hufanya shughuli zake kwa njia ya uwazi, umakini, bila mapendeleo na kwa lengo la kutekeleza haki ili umma uwe na imani na mahakama.

## OMBI LA KUJADILIANA KUHUSU KESI NI NINI?

Ombi la majadiliano kuhusu kesi ni maagano kati ya mshtakiwa na kiongozi wa mashtaka kuhusu kesi ya mshtakiwa. Maagano hayo lazima yawe kwenye maandishi.

Mshtakiwa anaweza fikia makubaliano na kiongozi wa mashtaka kuhusu kesi yake kwa njia zifuatazo:

- Adhabu ipunguzwe
- Shtaka lipunguzwe
- Mashtaka yapunguzwe. Kwa mfano: kiongozi wa mashtaka anaweza punguza kesi ya wizi wa mabavu iwe kesi ya wizi wa kawaida
- Hapa nchini Kenya, maagano ya malalamiko yanaongozwa na kifungu cha 137A-O cha Criminal Procedure Code (Plea Bargaining Rules, 2018)

## KIONGOZI WA MASHTAKA LAZIMA AHAKIKISHE YAFUATAYO YAMEZINGATIWA KABLA YA MAAGANO:

- Mshtakiwa amefahamishwa ya kwamba ana haki ya kuendelea na kesi mahakamani
- Mshtakiwa amefahamishwa ushahidi uliopo
- Maagano hayo in ya haki na kweli
- Mshtakiwa anaelewa kesi iliopo dhidi yake na amejitolea kufanya majadiliano
- Ana haki ya kutafuta mwakilishi
- Ameelewa vifungu vyote vilivyopo katika maagano hayo

## MSHTAKIWA

- Atakubali kwamba hataendelea na kesi
- Atakubali mashtaka dhidi yake kulingana na maagano
- Ako tayari kwa hukumu ya mahakama Hukumu ya mahakama yaweza kuwa: kifungu cha jela, faini, Kifungu cha nje, utumishi kwa jamii au kuomba msamaha
- Hawezi kata rufaa
- Akubali kwamba atashirikiana na wapelelezi wa kesi kwa njia ya kusaidia upelelezi ama kutoa ushahidi dhidi ya washtakiwa wengine. Asipofanya hivi, maagano hayo huenda yakakataliwa na mahakama

Illustrator: Paul Kelemba

## KIONGOZI WA MASHTAKA ANAFAA PIA:

- Kushauriana na wapelelezi wa kesi
- Kueleza walalamishi
- Kujifahamisha maoni ya waathiriwa au walalamishi





## KIONGOZI WA MASHTAKA BAADA YA MAAGANO:

- Anaweza ondoa mashtaka
- Anaweza punguza baadhi ya mashtaka
- Anaweza badilisha shtaka kwa kulipunguza
- Anaweza pendekeza hukumu




## MAHAKAMA

- Itazingatia maagano hayo
- Itahakikisha kwamba maagano hayo ni ya haki
- Itahakikisha kwamba haki za wathiriwa zimezingatiwa
- Uadilifu wa sekta ya haki umehifadhiwa



## UMUHIMU WA OMBI LA MAJADILIANO KUHUSU KESI

- Gharama ya kufanya kesi hupungua
- Huokoa muda
- Huwezesha viongozi wa mashtaka kutilia maanani kesi zilizo na uzito mahakamani
- Mshtakiwa huepuka adhabu ya juu



- Kesi kuchukua muda mfupi
- Hukumu zinazotolewa huwa zimepunguzwa. Kwa mfano, kifungo cha miaka tatu badala ya miaka saba
- Mshtakiwa anaweza hukumiwa bila kuenda jela
- Fidia kwa hasara
- Hupunguza idadi na msongamano ya wafungwa gerezani
- Hupunguza mrundiko wa kesi kortini
- Huimarisha kupata haki kwa mwananchi wa kawaida
- Huimarisha imani katika utekelezaji wa kesi za uhalifu nchini

## ASILIMIA YA OMBI LA KUJADILIANA KUHUSU KESI ULIMWENGUNI

**300%**

Asilimia ya ongezeko la majadiliano haya tangu 1990 (Fair Trials)

**97%**

Kesi zilizotatuliwa kwa njia hii nchini Marekani Kabla ya 2015

**64%**

Kesi zilizotatuliwa kwa njia hii nchini Urusi kabla ya 2014

## UNAHITAJI TAARIFA ZAIDI KUHUSU OMBI LA KUJADILIANA KUHUSU KESI?

### WASILIANA NA

**Afisi ya Mkuu wa Mashtaka ya Umma (ODPP)**
ODPP House, Ragati Road, Upper Hill
S.L.P. 30701-00100
NAIROBI
KENYA

Nambari ya simu: +254 2732090/2732240
Rununu: 0723202880/0787880580
Faksi: +254 2 2243524/2251808
Barua pepe: info@odpp.go.ke
Tuvuti: www.odpp.go.ke
T-@ODPP_KE

Funded by the European Union

UNODC
United Nations Office on Drugs and Crime

Brosha hii ilitolewa kwa msaada wa kifedha wa Jumuiya ya Ulaya. Yote yaliyomo yametolewa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma na hayaakisi maoni ya Jumuiya ya Ulaya.